OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI KASANGA,
S. L. P. 418
MAFINGA.
14/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI

_____

_____

UTANGULIZI
Napenda kukupongeza kwa kuchagulia kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari kasanga iliyopo Halmashauri ya Mufindi kata ya Kasanga Shule ya kasanga sekondari ipo umbali wa Km 1.5 kutoka Ofisi ya kata katika barabara itokayo Igowole kuelekea Udumuka - Kilolo.Shule ipo upande wa kulia barabarani.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KASANGA

i. KUFUNGUA SHULE
Shule itafungua tarehe 11/1/2021 na kila mwanafunzi atatakiwa afike shuleni siku hiyo bila kukosa akiwa na mahitaji yote ya shule kama ilivyoagizwa.

ii. MASOMO
Shule inafundisha masomo yafuatayo :Hisabati,Jiografia, Uraia. Historia, Biolojia, Kiswahili,Agriculture, Kiingereza, Fizikia, Kemia pamoja na somo la Dini ambalo kila Mwanafunzi atahudhulia vipindi vyake.Pia, tarehe hiyo mwanafunzi aje na faili gumu la kutunzia kumbukumbu zake pamoja na Daftari 11 kubwa (KAUNTA)

iii. SARE YA SHULE

a) WASICHANA

- Sketi mbili(2) rangi kijani kikavu. Sketi iwe ndefu ya kufunika viatu na yenye malinda 16 tu, sketi fupi haita kubaliwa
- Blauzi nyeupe, mikono mirefu na tai ya kijani kikavu.
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili(2)
- Soksi jozi mbili nyeupe.
- Sweta rangi ya kijani kikavu.
- Raba za michezo.
- T-shirt 1 rangi ya njano isiyo na maandishi yoyote pamoja na bukta ya blue

b) WAVULANA

- Suruali ya kijani kikavu mbili (2)
- Shart nyeupe mbili mikono mirefu.
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili (2)
- Sweta rangi ya kijani kikavu.
- Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
- Tai rangi ya kijani kikavu ndefu.
- Raba za michezo
- T-shirt ya njano isiyo na maandishi yoyote pampja na bukta ya blue.

NB:Raba,T-shirt pamoja na Bukta vitavaliwa Jumanne kwa kuwa ndiyo siku ya michezo

c) MICHANGO YA CHAKULA

Wazazi katika vikao vyao walikubaliana kuwa watoto wawe wanapata chakula shuleni wote. Hivyo nawe Mzazi/Mlezi ungana na wenzio kwa kutoa michango kama ifuatavyo:

1. Mahindi debe 2 Muhula wa I debe 1na Muhula wa II debe 1
2. Fedha taslimu shilingi 16,000/= zitalipwa kwa awamu tatu 5000, 5000,na 6000
3. Maharage lita 10.Awamu tatu.Lita 3 ,Lita 3,Lita 4

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa Viongozi Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu/kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa, kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
iv. Usafi wa mwili na mazingira ya shule.
v. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
vi. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
iv. Uvutaji bangi.
v. Makosa ya jinai.
vi. Kupigana na kupiga.
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
x. Kutoa mimba.

xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.

MAELEZO MENGINE MUHIMU

1. Inasisitizwa kwamba kila Mwanafunzi aje na MAHITAJI YOTE
2. Kila mwanafunzi anailazimika kutii na kuheshimu sheria zote za shule na taratibu zake.
3. Kila mwanafunzi itamlazimu kujifunza Wimbo wa shule, Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Tanzania.
4. Kila Mzazi/Mlezi na Mwanafunzi husika itamlazimu kujaza kiambatanisho 'A' kwa ukamilifu na kuleta shule mnamo tarehe _____
5. Pia kiambatanisho 'B' kiletwe shule mnamo tarehe _____
6. Tarehe 07/1/2021 mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa hii inapatikana mahakamani. Cheti cha kuzaliwa (Copy) ni lazima ulete.
7. Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria masomo yote kwa wakati uliopangwa bila kuchagua, bila kuchelewa.

NB: Kwa kuwa wazazi tumekuwa tukichanganya sare ya shule hiyo kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza mfike shuleni tarehe_____ kwaajili ya kuelekezana vizuri juu ya sare ya kamili ya shule ikiwa kama ulazima.

Ahsante

KARIBU KASANGA SEKONDARI

- SHULE YENYE MATUMAINI MAKUBWA NA MAENDELEO YAKO KITAALUMA, KIMICHEZO NA KIUTAMADUNI.
- SHULE ITAKAYO KUANDAA VEMA NA MAISHA YAKO YA BAADAE.

_____
NG'AMILO MS
MKUU WA SHULE

Kwa mawasiliano zaidi piga simu Namba +255 0764 325 730 au 0783 469 718

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
KITAMBULISHO 'B'

SHULE YA SEKONDARI KASANGA,
S.L.P.418,
MAFINGA

DAKTARI_____
HOSPITARI YA_____
S.L.P._____
_____

YAH: FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI.

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za Mzazi/Mlezi wake na uthibitishe kama utaweza kumudu masomo ya sekondari katika shule hii.

Ni muhimu kabla ya kuja hapa kujua Afya yake.

_____
NG'AMILO MS
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
_____ SEKONDARI,
MAFINGA,

YAH: MWANAFUNZI _____

Matokeo ya vipimo vya afya ya Mwanafunzi aliyetajwa hapo juu

1. Urine_____
2. Stool_____
3. HB_____
4. Pregnancy test_____
5. Spleen_____
6. Chest_____
7. Eyes_____
8. Ears_____
9. Physical abnormality _____
   _____
   _____
10. _____

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu

_____

_____

Ataweza/ Hataweza kumudu masomo ya sekondari

_____	_____	_____	_____
JINA LA DAKTARI	**CHEO**	**SAHIHI**	**TAREHE**

KIAMBATANISHO ‘A’

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

_____
_____
_____

TAREHE_____

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI _____
S.L.P.418,
MAFINGA.

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI _____

MWANAFUNZI:_____

KIDATO_____MWAKA_____

1. Mimi_____
mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliye tajwa hapo juu nakiri kuwa nimeelewa maelezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.

2. Nakubali mwanangu ajiunge na shule hii na nitatekeleza yale yote yanayo nihisu kwangu.
3. Wakati wake, kama ilivyo agizwa kwenye maelezo ya kujiunga na shule.
4. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufanikisha malengo yake.
5. Ya kujiunga na shule hii
6. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo shuleni

JINA LA MZAZI/MLEZI_____SAHIHI_____
ANWANI YA MZAZI/MLEZI_____
NABA YA SIMU_____

Mimi_____
Niliye chaguliwa kujiunga na shule hii, naahidi kuwa mtiifu kwa sheria za shule kuwa na nidhamu ya kujituma kusoma kwa bidii na kuwa mfano bora kwa wanafunzi wenzangu ili nifikie malengo ya shule hii. Tofauti na haya niondolewe shuleni mara moja.

JINA LA MWANAFUNZI_____
SAHIHI_____
TAREHE_____